# *Waomba chuo chao cha Veta kufunza ufugaji *

Na Mariam Juma, Simanjiro

WANANCHI wa Kijiji cha Lebosoit A kilichopo Kata ya Eboret, Wilaya yaimanjiro mkoani Manyara, wameiomba serikali kuongeza fani ya ufugaji katika chuo kipya cha ufundi stadi (Veta) kilichojengwa katika kijiji hicho.

Walitoa ombi hilo wakati wa makabidhiano ya awamu ya pili ya mwendelezo wa ujenzi wa chuo hicho na vifaa kutoka mashirika ya Eclat Foundation la Tanzania, Der, Upendoociety kutoka Ujerumani ambapo ujenzi uligharimu zaidi yah milioni 675.

Jacob Laizer mkazi wa kijiji hicho alisema wanashukuru kwa kujengewa chuo lakini wao kama wafugaji wanaona bado kuna haja zaidi ya kuongezwa fani ya ufugaji.

"Sisi bado hatujajua ufugaji wa kisasa ambao utaleta tija kwetu, tungeletewa fani ya ufugaji ambayo italenga kutuelimisha jinsi ya kutibu mifugo, kulisha malisho bora kwa mifugo yetu na utunzaji wa mifugo ingetukomboa," alisema Laizer.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Charles Makongoro alisema yote hayo yasingewezekana kama wananchi hao wasingejitolea kutoa eneo lao lakini kwa kuwa wanatambua umuhimu wa elimu na fursa zinazotokea kwenye maeneo yao wameweza kukimbilia fursa hiyo kwa ajili ya watoto wao.

Alisema mafunzo ya ufundi stadi ni muhimu kwani ndiyo yanayozalisha watendaji wa kazi viwandani na sehemu nyingine za huduma za uzalishaji, mafundi stadi ndio rasilimali ya watu wanaohitajika zaidi kwani hata kimataifa uwiano wa chini unaeleza kuwa kwa kila mhandisi mmoja anatakiwa kufanya kazi na mafundi stadi wasiopungua 25.

Naye Mbunge wa Jimbo laimanjiro, Christopher Oleendeka alisema ni wakati wa Wanasimanjiro kujitokeza kwa wingi ili kuweza kunufaika na fursa hii ambayo itawakomboa vijana wa eneo hilo.

Alisema wakazi wengi waimanjiro ni wafugaji hivyo ingekuwa ni vyema fani ya ufugaji ambayo inatoa namna ya kutunza mifugo na kutibu mifugo wakazi wengi wa eneo hilo wangejitokeza.

Naye mfadhili kutokahirika la Upendoociety, Dk Fred Heimbach aliwaomba Veta kuendelea kushirikiana nao ili kuweka mwelekeo mzuri wa miradi hiyo huku akiwataka wananchi na wanafunzi kutumia vizuri vifaa vilivyopo na majengo ili viendelee kuwanufaisha na wengine.

Scanned with CamScanner

# Wanawake wafugaji wawezeshwa kiuchumi

Janeth Mushi, Mwananchi
jmushi@mwananchi.co.tz

Ngorongoro. Kuanzishwa kwa mabaraza ya haki ya wanawake wilayani Ngorongoro, mkoa wa Arusha, kunatajwa kusaidia wanawake kupata haki zao, ikiwamo kumiliki ardhi na kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Mabaraza hayo yaliyoanzishwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Pastoral Women Council (PWC), yanatajwa kuchangia kukua kiuchumi kwa wanawake wilayani humo baada ya kuanzishwa vikundi vya kuweka na kukopa fedha (Vicoba) na kupewa mitaji ya kuanzia miradi mbalimbali.

Wakizungumza juzi wakati wa ugawaji wa kondoo 168 kwa wajumbe wa mabaraza saba, wajumbe hao walisema elimu wanayoitoa kwenye jamii kupitia majukwaa mbalimbali yamesaidia wanawake kuelewa haki zao, ikiwemo ya umiliki wa ardhi.

Mmoja wa wajumbe hao kutoka kijiji cha Oloipiri, Maria Samora alisema kupitia mradi huo wamepata elimu inayowasaidia kujua haki zao ambazo walikuwa wakizikosa kutokana na mila na desturi potofu iliyokuwa imejengeka kwenye jamii.

"Kuhusu vitendo vya ukatili wa kijinsia tumeendelea kufundisha jamii ambayo kwa sasa inatupa ushirikiano, hasa kupinga ndoa za utotoni, tumevunja ndoa za utotoni nyingi kwa watoto wadogo wa kike," alisema.

Naye Taleng'o Lesoko alisema awali mila na desturi potofu zilikuwa zinachangia wanawake kushindwa kuendelea, huku jamii ikiamini watoto wa kike hawana haki ya kupata elimu.

Alisema ulishamiri mfumo dume uliokuwa ukikandamiza wanawake, hawakuwa wanasikilizwa na wanaume katika jamii hiyo ya kifugaji, sasa hali imeanza kubadilika baada ya wanaume kushirikishwa katika mabaraza yao.

"Mabaraza haya ya haki yamesaidia wanawake na wasichana, tumejengewa ujasiri wa kujitetea, tunafanya kazi na jamii ambapo ikitokea mtoto wa kike anaozeshwa akiwa na umri mdogo wanakimbilia kwetu na tunasaidia kuhakikisha ndoa hiyo haifungwi," alisema Lesoko.

> **'Tumeona tuwape wajumbe hawa mifugo badala ya pesa kwa sababu kwa jamii ya wafugaji mifugo ina thamani zaidi kuliko pesa.'**
>
> Mratibu wa mradi wa usawa kutoka PWC, Timothy Ole Yaili

Akizungumzia ugawaji wa kondoo kwa mabaraza hayo, Mratibu wa mradi wa usawa kutoka PWC, Timothy Ole Yaili alisema kondoo hao ni sehemu ya 528 watakaogawanywa katika wilaya hiyo na ya Longido ambao wana thamani ya Sh63 milioni.

Alisema lengo la kutoa mifugo hiyo ambapo kila mjumbe atapata kondoo mmoja ni motisha ili wapate ari na nguvu zaidi ya kufanya kazi hiyo ya kusaidia jamii.

"Tunagawa kondoo jike hawa 168 kwa mabaraza saba yenye wajumbe 24 kila baraza katika tarafa hii ya Loliondo ili kuwapa motisha zaidi, kwani wanaripoti matukio yanayofanyika katika jamii ambayo hayakuwa yakiripotiwa awali," alisema.

Alisema mabaraza hayo yaliyoanzishwa mwaka 2019, yalijengewa uwezo kupitia wataalamu mbalimbali ambapo wamewezа kuokoa watoto wa kike waliokuwa wanaozeshwa katika umri mdogo.

"Wanawake hawajawahi kumiliki ardhi katika historia ya jamii hii ya kifugaji, lakini sasa kupitia haya mabaraza wanamiliki, mbali na kuanzisha mabaraza pia tulianzisha Vicoba zaidi ya 400 na kuwapa mitaji ya Sh milioni moja kila kimoja," alisema.

Awali, Katibu Tawala wa wilaya ya Ngorongoro, Lemuel Kileo aliwapongeza wadau hao kwa kutekeleza miradi mbalimbali wilayani humo na kuyataka mashirika mengine yasiyo ya kiserikali kuiga mfano huo kwa kusaidia jamii badala ya kujihusisha na migogoro katika jamii.

Scanned with CamScanner